TANGAZO LA SERIKALI Na. 118 la tarehe

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA 355)

**AMRI**

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA NYAMILANGANO YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Nyamilangano ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya Mipaka ifuatavyo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 403 yenye majira - nukta 427203MS,9542737KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ22°30'50"MS kwa umbali wa kilomita 4.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 379 yenye majira - nukta 428831MS, 9546608KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ37°23'22"MS kwa umbali wa kilomita 3.88 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 370 yenye majira – nukta 431213MS, 9549730KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ00°16'16"MS kwa umbali wa kilomita 1.27 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 369 yenye majira – nukta 431280MS,9550947KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ49°50'54"MS kwa umbali wa kilomita 2.58 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 324 yenye majira - nukta 433211MS,9552620KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KS86°54'42"MS kwa umbali wa kilomita 11.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 311 yenye majira – nukta 445136MS, 9551997KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS65°42'27"MS kwa umbali wa kilomita 1.24 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 312 yenye majira - nukta 446276MS,9551472KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS09°51'03"MS kwa umbali wa kilomita 1.82 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 394 yenye majira - nukta 446584MS, 9549708KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika ueleekeo wa KS49°47'26"MS kwa umbali wa kilomita 2.87 hadi kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba SHV 396 yenye majira - nukta 444394MS,9547823KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS49°47'26"MG kwa umbali wa kilomita 10.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 306 yenye majira - nukta 447353MS,9538150KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS17°07'10"MS kwa umbali wa kilomita 14.07 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 431 yenye majira – nukta 435486MS,9530844KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS58°37'16"MG kwa umbali wa kilomita 3.82 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 455 yenye majira - nukta 434398MS, 9534428KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KS16°30'01"MG kwa umbali wa kilomita 10.hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*